



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI



S.L.P. 400, Babati. Email  
ded@babatidc.go.tz info@babatidc.go.tz  
Website: www.babatidc.go.tz

**TANGAZO LA MAJINA YA MIPAKA YA VIJILI NA VITONGOJI KWA  
AJILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024.**

*Limetolewa chini ya kanuni ya 5 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji za mwaka 2024 (Tangazo la serikali Na 571/2024)*

Kwa mujibu wa Kanuni ya 5 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji, za mwaka 2024, Tangazo la Serikali namba 571, la mwaka 2024, Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati kwa kuzingatia amri ya mgawanyo wa maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa ( Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 2024, Tangazo la Serikali namba 796/2024 ambayo ni Amri ya mgawanyo wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) iliyoainisha orodha ya Vijiji na Vitongoji anawatangazia wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati majina ya maeneo na mipaka ya kila Kijiji na Kitongoji yatakayoshiriki katika Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, Wajumbe wa viti maalum na Mwenyekiti wa Kitongoji katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe **27/11/2024**.

Orodha ya majina ya Vijiji na Vitongoji kwa Kata husika imeambatanishwa pamoja na Tangazo hili.

Anna Mbogo

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI  
16/09/2024**